# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb Na: HWP/I.10/32/VOL.V/47** **10/05/2023**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma chenye **Kumb. Na. FA.97.170/36/01"C"/05** cha Tarehe **03 Mei 2023.**

Aidha, Nafasi ya Msaidizi wa kumbukumbu II nafasi (1) , Mwandishi Mwendesha Ofisi II nafasi (1) na Dereva II nafasi (1) zitajazwa kupitia Tangazo lililotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani la Tarehe **13/04/2023** kwa kibali **Kumb. Na. FA.97/228/01"TEMP"/06** cha Tarehe **06 Aprili 2023.** Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kuomba nafasi za kazi kama inavyooneka kwenye Tangazo hili.

1. **MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III TGS. B (NAFASI 2)**

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form IV) au Kidato cha sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti **(NTA level 5)** katika moja ya Fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III**

- Atakuwa Mtendaji na Mshauri Mkuu wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika kupanga Mipango ya Maendeleo na utekelezaji wake.
- Atakuwa Afisa Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia Mapato na Matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- Atakuwa Mlinzi wa Amani na Utawala Bora katika Kijiji
- Atakuwa Katibu wa Serikali ya Kijiji

- Atatafsiri Sera, Taratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji
- Ataratibu na kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Sharia ndogo za Kijiji
- Ataratibu na kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuwasilisha kwenye Halmashauri ya Kijiji na baadae kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji na Kata
- Ataratibu Vikao vya Maendeleo ya Kijiji vitakavyowahusisha Wananchi na Wataalamu waliopo kwenye eneo lake.
- Atasaidia katika Mikakati mbalimbali ya kuondoa Njaa , Umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- Atasimamia na kuratibu matumizi bora ya nguvu kazi katika Kijiji.
- Atasaidia ukusanyaji wa kumbukumbu za walipa kodi , Wataalam mbalimbali na NGO's zilizopo kwenye Kijiji

**MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI WA NAFASI YA KAZI**

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo:

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania
- Waombaji wote wawe na umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Waombaji wote waandike barua zao za maombi wenyewe kwa mkono na aambatanishe Wasifu (CV), Vivuli vya Vyeti vyake vya Taaluma na Ujuzi, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili za ukubwa wa Pasi ya kusafiria (Passport) size za hivi karibuni.
- Waombaji wote wawe na Namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika mazingira ya vijijini.
- Waombaji wenye vyeti vya kidato cha Nne cha Taaluma ambao vimepatikana nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) NA Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).
- Waombaji waliofukuzwa Kazi, kupunguzwa au kuachishwa kazi katika Utumishi Wa Umma hawaruhusiwi.
- Waombaji ambao hawana sifa wanashauriwa kutokuomba kwa sababu barua zao hazitashughulikiwa
- "Testmonial", "Provisional statement" hati ya matokeo ya kidato cha Nne,Sita na Result slip hazitapokelewa.
- Watakaochaguliwa kufanya Usaili watajulishwa Tarehe ya usaili.

- Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **16 Mei 2023** Saa Tisa na nusu Alasiri **(09:30)**
- Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Pangani,**
**S.L.P. 89,**
**PANGANI.**

- Pia Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani www.panganidc.go.tz
- Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma www.ajira.go.tz.
- Mbao za Matangazo

**Isaya Mbenje**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**PANGANI**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
PANGANI

Nakala; Katibu
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM)
Eneo la Dkt Asha Rose Migiro,
Sanduku la Posta 2320
**DODOMA**

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe: ded@panganidc.go.tz, Tovuti: www.panganidc.go.tz